

1. Utangulizi

Serikali ya Tanzania iko kwenye jitihada za kubadili Tanzania kuwa ya viwanda ili kufanya kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo 2025 kama ilivyo ainishwa kwenye Dira ya Maendeleo ya 2025. Pamoja na kua na jitiada nyingi za serikali zinazolenga kuyafikia malengo hayo kupitia maendeleo katika sekta binafsi, bado changamoto nyingi zimeendelea kuwa kikwazo

Kwa mfano hakuna ujumbe halisi na wazi kwa wawekezaji wa ndani na wa nje unaoelezea ni jinsi gani hasa maendeleo haya ya viwanda yatafiikiwa.

Maendeleo ya viwanda na uendelezaji wa viwanda vya vipaumbele umeainishwa lakini mgongano wa sera na kanuni katika maeneo mengi bado umeendelea kuwa changa moto, maeneo kama ya usajili wa bishara, kodi, ardhi, huduma za kifedha na mazingira ya ndani kwa ujumla na kadhalika.

Pia viwanda vikubwa vimekuwa vikiendelea kukua lakini upande mwingine viwanda vidogo vidogo vimekuwa havikui kwa kasi inayoridhisha wakati huo huo makundi makubwa ya viwanda yakifumuka kutoka katika maeneo mengine. Upatikanaji wa fedha, usimamizi wa biashara na kuongeza ubora na ufanisi yamebakia kuwa moja ya matatizo yanayoyakabili makampuni machanga, madogo na ya kati.

Ili kuweza kuzitatua hizo changamoto, na kukuza zaidi "viwanda" ambayo ndio ajenda kuu ya mpango wa pili wa maendeleo wa taifa la Tanzania, Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA) limekuwa likisaidia maendeleo ya sekta za uchumi kulingana na vipaumbele vifuatavyo:-

1. Kuwasilisha sera ya viwanda yenye uwazi na uhalisia
2. Kuhakikisha mazingira yasiyokinzana na sera na
3. Kujenga sekta kibinafsi yenye nguvu

Zaidi sana, msaada kutoka Japani umeegemea zaidi kutokana na uzoefu iliyonayo katika maendeleo ya viwanda kama ilivyoelezwa hapo chini katika mradi wa KAIZEN.

2. Uzalishaji na Uboreshaji Kitaifa: KAIZEN

"KAIZEN" ni neno la Kijapani, likimaanisha "Uboreshaji". Ni falsafa ya usimamizi na ujuzi unaotengenezwa nchini Japan kwa ajili ya kuboresha ubora wa mashirika na makampuni. KAIZEN ni mbinu ya kibinadamu inayoimarisha kazi ya timu, kujitegemea, ubunifu na ujuzi. Ingawa KAIZEN ni njia ya muda mrefu yenye hatua ndogo na kwa uwekezaji mdogo, inalenga uwezo wa msingi wa makampuni kama uzalishaji na usimamizi, ambao ni muhimu kwa ukuaji wa makampuni.

"Mradi wa Kuimarisha Biashara ya Viwanda kwa Kuboresha Ubora na Uzalishaji" (unaojulikana kama "Mradi wa KAIZEN") ulianza mwezi wa Aprili 2013, una lengo la kuelezea harakati za KAIZEN na kutanua wigo nchini Tanzania. Mradi huo ulifanyika na Kitengo cha KAIZEN Tanzania (TKU) kilichoanzishwa katika Wizara ya Viwanda na Biashara (MIT), kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Viwanda vidogo (SIDO) na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE).

Mradi umeanzisha sera itwayo "Mkakati wa Sera za Kazi za Kukuza Mbinu za KAIZEN Tanzania 2016-2025" na inatoa huduma za ushauri wa KAIZEN wa moja kwa moja. Kati ya Makampuni / Mashirika mia moja (100) hadi sasa, ishirini nasita (26) ni wakufunzi wa ngazi za juu waliobobea (Advanced Trainers) wa KAIZEN na walithibitishwa na Wizara ya Viwanda na Biashara. Aidha, zaidi ya Makampuni mia moja (100) ni wakufunzi hasa wa ngazi za juu waliobobea katika KAIZEN na kutarajia kutunukiwa vyeti. Inatarajwa kwamba wakufunzi wa KAIZEN watasambaza elimu ya KAIZEN kwa makampuni na mashirika mbalimbali na kupanua wigo wa KAIZEN kwa maeneo



Kabla



Baada

Kabla / Baada ya kutekeleza KAIZEN (mfano wa "5S")

meni nchini Tanzania. Kwa mfano, kampuni moja ya Arusha imetekeleza KAIZEN kwa msaada wa mradi huu, na imeweza kupunguza kiwango cha taka (Polyethilini) kutoka asilimia 6.4 hadi asilimia 3.6, na hivyo kufanikiwa kuokoa Tsh 50,000,000 kwa mwezi. Aidha, kampuni hiyo iliongeza uzalishaji (kwa kila mashine ya extruder kwa siku) kutoka kilo 345.7 hadi kilo 455.6 ambayo ina maana zaidi ya asilimia 30 ya uboreshaji wa tija.

Viwanda vidogovidogo vingine huko Moshi vinatekeleza "5S" (moja ya mbinu za KAIZEN) kwa kutumia maneno "5S", yaani; Sasambua, Seti, Safisha, Sanifisha na Shikilia/ Dumisha), na mbinu hiyo inapunguza muda wa kutafuta zana zinazo hitajika kutoka dakika 15 hadi sekunde 47 tu, hii imweza kupunguza muda kwa asilimia 95 na hivyo kuchangia katika kuboresha uzalishaji.

Huduma ya KAIZEN imepanuka kutoka SIDO na CBE hadi EPZA, Serikali za Mitaa (Mamlaka za Serikali za Mitaa), Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (VETA), Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, mabanki, washauri binafsi, nk. Tunategemea kupanua harakati za KAIZEN Tanzania katika viwango na maeneo mbalimbali, na kuchangia kukuza si tu katika sekta ya viwanda lakini pia katika sekta zote.

3. Maendeleo ya Kongano

"Huwa tunajadiliana na kubadilishana taarifa/mawazo, juu ya umuhimu wa mashine (grading machine). Kuna uwezekano pia kupokea oda kubwa na kugawana kati yetu, na tunagawana wateja baina yetu pale ambapo mtu anapona havezi," anasema mjumbe wa Kongano la Mpunga kutoka Mbeya. Maendeleo ya Kongano ya Viwanda huvutia watu nchini kama njia ya maendeleo ya kukuza uchumi wa viwanda. "Kongano ya Viwanda" imetafsiriwa na Profesa Michael Porter kutoka Chuo Kikuu cha Harvard kama ifuatavyo: "Vikundi, kampuni na mashirika vilivyo karibu kijografia na tasnia zenye bidhaa zinazo fanana na kushabiana". Kulingana na wazo hili, JICA imesaidia SIDO tangu mwaka 2011 ili kukuza na kutekeleza "Maendeleo ya Kongano".

Moja ya mafanikio ya kongano yameibuka katika Wilaya ya Singida, ambapo kongano ya alizeti imeanzishwa na inaendelea sehemu hiyo katika kijiji cha Mtinko. Kongano hilo lina wanachama zaidi ya 100 sasa, ambao ni wakulima, wasindikaji na wasafirishaji. Kwa nguvu zao wenyewe, wameweza kuvutia taasisi mbalimbali na kusaidia.



Mafunzo ya Kaizen

Kongano, wameweza kufungua ghala na mashine ya kusafisha mafuta ya alizeti. Wadau wa kilimo, wameweza kusambaza mbegu kwa wanachama wa kusindika, na wameweza kuyasafisha mafuta machafu yakawa masafi. Mwanachama wa Kongano anasema, "Tunaweza kujaribu kuzalisha na kununua mbegu za alizeti zaidi bila kuhangaika kuuza mafuta yasiyo masafi. Kongano hutusaidia kuja pamoja ili tuelewe fursa zaidi. Mtinko sasa inajulikana zaidi kati ya viongozi wa serikali za mitaa kuliko hapo awali"

Kiasi cha mbegu za alizeti katika Wilaya ya Singida kiliongezeka zaidi ya mara mbili kwa miaka 4, yaani kutoka tani 4,407 (mwaka 2012) hadi tani 10,792 (mwaka 2016). Kwa jitihada za ushirikiano, mbegu zaidi zinaweza kutumiwa kwa njia ya mzunguko wa thamani (a coordinated value chain) unaohusishwa na kuleta faida zaidi kwa wanachama wa Kongano.

Kwa msaada wa JICA, SIDO inaandaa mwongozo wa uendeshaji wa Kongano. Wadau wa maendeleo ya Kongano nchini Tanzania wanaweza kutumia ili kuanzisha na kukuza maendeleo ya Kongano katika maeneo yao

4. Kukuza ukuaji wa uchumi: Mradi wa kujenga uwezo katika kuboresha biashara na udhibiti wa mipaka katika Afrika mashariki

Mamlaka tano za mapato katika Afrika Mashariki, yaani, Tanzania, Burundi, Kenya, Rwanda na Uganda, kwa kushirikiana na JICA zimekuwa zikitekeleza mradi wa ushirikiano wa kiufundi unaojulikana kama mradi.

na kujenga uwezo katika kuboresha biashara na udhibiti wa mipaka katika Afrika mashariki tangu Desemba 2017. Lengo la mradi huu ni kuhakikisha kwamba kunakua na tija kwenye vituo vya forodha katika mipaka iliyolengwa na mradi lakini pia kujenga uwezo katika usimamizi wa viashiria hatari katika forodha na uthibiti mipakani katika Afrika Mashariki

Ili kuimarisha biashara ndani na nje ya Afrika Mashariki, JICA imekuwa ikiunga mkono na kufadhili uanzishwaji wa vituo vya forodha (One Stop Border Post) vilivyopo Rusumo, kati ya mpaka wa Tanzania na Rwanda, na Kingine kilichopo Namanga, mpakani mwa Tanzania na Kenya. Kupitia msaada huu ambao ulilenga hasa kujenga na kuboresha miundombinu pamoja na kutoa mafunzo ili kuboresha taratibu za utoaji mizigo katika vituo hivi, muda wa kutoa mizigo katika kituo cha Rusumo umepungua kwa asilimia 73, kutoka saa 8 na dakika 42 hadi masaa 2 na dakika 20 tu.

Pia vituo hivi vya forodha vimechangia kuongeza idadi ya malori yanayopita kwenye mipaka hii na kuongezeka kwa kiwango cha biashara kinachopita kwenye mipaka hii. Msaada huu pia umechangia kurahisika kwa usimamizi wa mipaka na kurahisisha mtiririko wa biashara baina ya nchi husika.

Rais Magufuli alipongeza juhuhu hizi na kusema vituo hivi vya kisasa vya forodha mipakani vinaonyesha kuwa "umoja ni nguvu".

Ushirikiano kati ya mamlaka za mapato Afrika Mashariki na JICA ulianza tangu mwaka 2007 pindi awamu ya kwanza ya

mradi huu ilipoanza na sasa mradi huu uko katika awamu yake ya nne, ukiangazia zaidi juu ya udhibiti mipakani, sawa sawa na matamshi ya wakuu wa mataifa ya Afrika ambao waligusia juu ya umuhimu wa maendeleo ya kiuchumi na usalama kwa maendeleo endelevu ya Afrika.

Katika Mradi huu, JICA inafanya kazi kwa karibu na Shirika la Forodha la Dunia (WCO) na Taasisi ya Forodha ya Japan katika kutoa mafunzo ya kujenga uwezo wa forodha ili kuimarisha biashara na udhibiti wa mipaka katika eneo hili la Afrika mashariki. Hadi sasa, Mradi umeweza kutengeneza wakufunzi zaidi ya 90, ambao ni wafanyakazi katika ofisi mbalimbali za forodha katika kanda hii ya Afrika Mashariki ambao wametoka katika maeneo ya hesabu, Uchambuzi (HS classification) na uchambuzi wa kiintelliginsia hii imefanyika ili kujenga uwezo endelevu wa kikanda wa utoaji mafunzo. Aidha zaidi ya maafisa na mawakala wa utoaji mizigo 3,000 wamepatiwa mafunzo.

5. Maendeleo ya Sekta Binafsi: Mradi wa Sola (Off-Grid Solar Power Project by WASSHA Inc.)

Idadi ya watu duniani ilikuwa takribani bilioni 7.3 mwaka 2016 na bilioni 1.2 ni adadi ya watu waishio bila umeme. Asilimia 67 ya watu Tanzania hawana umeme (Benki ya Dunia, 2016). Watu wengi wanatumia mafuta ya taa na taa za chemli au koroboi kutatua matatizo ya nishati ya umemena hivyo husababisha moto katika makazi yao na hata kuumwa vifua. WASSHA Inc ni kampuni ya Kijapani inayodhamiria kutatua changamoto ya umeme kwa kukodisha taa za sola katika makazi ya watu.

Kampuni ya WASSHA ilizinduliwa mnamo mwaka 2015 na sasa ina wahudumia wateja takribani milioni 1.5. Kupitia huduma za WASSHA, watu wanaweza kutumia taa za kukodisha kwa sababu zina mwanga mkali, bei rahisi na ni salama kuliko koroboi. Hata hivyo watu wanaweza kunufaika zaidi kwa mfano, watu wanaweza kufungua maduka kwa kukodisha taa hizi na kuongeza kipato. Aidha watoto wanaweza kutumia kusomea na hata kuchaji simu kwa kutumia taa hizi.

WASSHA wanatoa huduma za kufunga paneli za jua (solar panels) na vifaa vingine katika duka na kumwezesha mwenye duka kuwa na uwezo wa kuhudumia wateja 30 kwa kuchaji taa zao na kebo (Cables) za kuchaji simu. Wenye maduka wanaweza kuanza biashara hii bila gharama zozote za awali.

Pia wana uwezo wa kufanya malipo kwa WASSHA kwa kupitia simu na kupata namba za siri na kuwawezesha kuendelea kutoa huduma kwa wateja.

WASSHA wamejitanaa kutoa huduma zao kwa maduka 900 ndani ya mikoa 13 nchini, pia wana mkakati wa kuenza zaidi huduma zao barani Afrika na hata bara la Asia.

Dhima ya kampuni ni "power to the people". Kupitia maduka, WASSHA wameleta uzoefu mpya kwenye upande wa sola ambao ni rahisi kwa gharama, rahisi kupatikana na ni salama. WASSHA wana amini nchi inaweza kuendelea kwa kupitia njia zake na hakuna ulazima wa kupitia njia za mataifa mengine. Kwa maneno mengine, nchi za Afrika zinaweza kutumia utamaduni wao kusukuma maendeleo kwa njia ya teknolojia ya kutuma pesa kwenye simu za viganjani.

WASSHA inamatumaini kuwa mstari wa mbele katika jamii kwa biashara ya umeme wa sola kwa kupitia mtandao wake wa maduka. JICA imekuwa mstari wa mbele kusaidia mradi huu kama Mshirika Mwenza wa WASSHA Inc tangu mnamo mwaka 2016. Ilikuwa mara ya kwanza kwa JICA kusaidia sekta binafsi kwa kuwezesha fedha katika ukanda wa Nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara. JICA inaamini ukuaji wa WASSHA utaleta maendeleo ya kiuchumi katika jamii ya Kitanzania kwa kutoa huduma nafuu za umeme wa sola kwa kukodisha kwa wananchi taa hizo hususani vijijini na kutengeneza ajira.



wanasingida wakifurahia mafuta ya alizeti.

6. Kuboresha kuaminika kwa bajeti: mradi wa kujenga uwezo wa ukaguzi wa ndani awamu ya 2

"Kwa ujuzi na maarifa ya ukaguzi wa ndani unaoangalia viashiria hatari, (risk base internal audit) Mabingwa katika ukaguzi wa ndani wamesaidia tasisi yetu kuimarisha, kuepuka na kudhibiti hatari kupitia kuundwa kwa nyaraka zinazoelezea maeneo hatarishi, nyaraka kama (risk register na Risk management framework).

Aidha, Mabingwa wa ukaguzi wa ndani pia walitoa mafunzo ya ndani kwa wafanyakazi wanaofanya kazi kwenye maeneo hatari zaidi ikijumuisha maofisa wa ngazi za juu, kwa kufanya hivyo shirika limeweza kuokoa zaidi ya Tsh 12 milioni ambazo zingeweza kulipwa kwa washauri wa nje kwa ajili ya kufanya tathmini ya viashiria hatari kila mwaka, lakini muhimu zaidi, ni kwamba sasa taasisi yetu imeweza kujiandaa kukabili uwezekano wa matukio hatari katika kazi za ujenzi barabarani ambayo yanaweza kuathiri maendeleo ya miundo mbinu nchini" (nukuu ya Bw. Jonas Jackson, bingwa wa ukaguzi wa ndani kutoka TARURA, Dar es salaam).

"Taasisi yetu ya ukaguzi wa ndani iliona kuna mapungufu kwenye usimamizi wa mapato ambayo ilikua inaumiza sana taasisi yetu. Kitengo chetu kilipendekwa kwa uongozi kuwekwa kwa udhibiti zaidi na wa mara kwa mara kama vile mashine za kielektroniki ili kuweza kujua mapato yanayolingia katika mfumo wa ukusanyaji mapato wa serikali za mitaa ili kuweza kugundua mapungufu/ hitilafu kweye ukusanyaji mapato ndani ya muda mfupi. Matokeo yake, halmashauri imeweza kupunguza ufujaji wa mapato na hivyo kupelekea mapato ya halmashauri kuongezeka kwa zaidi ya asilimia 60, zaidi ya lengo lake la mwaka katika kipindi cha miezi sita tu, hii imekuwa ni kumbukumbu ya kihistoria" (nukuu ya Bw. Pascal Jgadi, Bingwa wa Ukaguzi wa ndani kutoka Halmashauri ya wilaya ya Musoma).


Umuhimu wa ukaguzi wa ndani katika serikali Tanzania umeongezeka zaidi hasa wakati wa kipindi hiki wakati serikali inatekeleza mpango wa pili wa maendeleo amabao umelenga kuifanya nchi kuwa ya uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025, ili kufikia lengo hili ufanisi, tija na uwazi katika matumizi ya mapato ya serikali ni muhimu sana ili utekelezaji wa mpango huu uweze kufanikiwa, hivyo kazi za ukaguzi wa ndani katika kila taasisi ya serikali ni muhimu sana Tangu uteuzi wa mkaguzi wa ndani na kuanzishwa kwa kitengo cha ukaguzi wa ndani chini ya wizara ya fedha mnamo mwaka 2011, kitengo hiki cha ukaguzi wa ndani kimekuwa kinara katika kuongoza taasisi za serikali katika kuboresha uthibiti wa ndani, usimamizi, na usimamizi wa viashiria hatari kupitia kazi za ukaguzi wa ndani JICA imekuwa ikitoa msaada wa ushirikiano wa kiufundi kwa wizara ya fedha tangu mwaka 2009, kupitia mradi huu wa kuwajengea uwezo wakaguzi wa ndani, ili kuboresha kazi za ukaguzi wa ndani katika serikali ya Tanzania.

Mradi umetengeneza nyenzo za ukaguzi ambazo ziko katika seti ya vitabu vidogo vya mkaguzi wa ndani na kuwafanyia mafunzo ya kuwafanya wakaguzi wa ndani kuwa mabingwa katika ukaguzi wa ndani, ambao pia mabingwa hawa wamekuwa wakutumika kama wakufunzi kwa wenzao kupitia mafunzo kazini.

Tangu kuanziashwa kwa programu ya mabingwa wa ukaguzi wa ndani mnamo mwaka 2017, mpaka leo mradi umeweza kutengeneza mabingwa wa ukaguzi wa ndani wapatao 80 kutoka taasisi za umma 57. Mradi pia umeweza kuchangia kuimarisha ujuzi kwa wakaguzi wa ndani ikiwa pia ni pamoja na kuimarisha taratibu



Sherehe za Ufunguzi wa kituo cha forodha cha Namanga




Seti ya vitabu vya ukaguzi wa ndani

na nyaraka za kufanyia ukaguzi katika kiwango kinachokubalika na kupitia matumizi ya aina ya ukaguzi unaoangazia viashiria hatari (risk based internal audit) ambao ulitambulishwa kwenye seti ya vitabu vidogo vya mkaguzi wa ndani Ofisi ya mkaguzi wa ndani kwa ushirikiano na JICA imekuwa ukiendeleza programu hii ya kuthibitisha mabingwa wa kaguzi za ndani kwa kuongeza

idadi ya wakaguzi bingwa katika taasisi za serikali, mabingwa hawa wanategemewa kuimarisha ukaguzi wa ndani na kuchangia katika mabadiliko katika taasisi za umma katika kuongeza uwajibikaji na uwazi katika matumizi ya rasilimali za umma na mapambano dhidi ya rushwa ambayo ni muhimu kwa maendeleo endelevu.



Watoto wakifurahia umeme wa sola



Kabla



Baada

Kabla

Baada



Duka la WASSHA

7. Uimarishaji wa Ukusanyaji wa Mapato: Mradi wa Kujengea Uwezo Mamlaka ya Mapato ya Tanzania

Tangu mwaka 2017 JICA kwa kushirikiana na mamlaka ya mapato Tanzania imekuwa ikitekeleza mradi wa kujengea uwezo mamlaka hii ya mapato ili iweze kutoa mafunzo yahasianayo na kodi kwa wafanyakazi wake. Madhumuni ya mradi huu ni kuboresha uwezo wa wafanya kazi wa mamlaka hii (TRA) katika ukusanyaji wa kodi, kupata ujuzi sahihi kutawezesha wafanyakazi wa TRA kusimamia ukusanyaji wa kodi kwa usahihi na kutoa huduma bora kwa walipa kodi.

Kwa sasa TRA inapitia katika kipindi ambacho wafanyakazi wake wengi wenye utajiri mkubwa wa ujuzi wanastaafu kiasi kikubwa hivyo suala la kukuza ujuzi kwa waajiriwa wapya kiasi cha

kufikia ujuzi wa wale wanaoondoka ni suala la haraka sana.

Mradi huu utatelezwa mpaka mwaka 2020, utagusa maeneo makubwa matatu kwa ajili ya kuboresha uwezo wa wafanyakazi wa TRA kama ifuatavyo:- Oneo la kwanza, linahusisha uboreshaji wa uwezo wa usimamizi wa kodi kwa wafanyakazi wa TRA kupitia utekelezaji wa mafunzo kutoka chuo cha usimamizi wa kodi Eneo la pili linahusisha juu ya kusaidia uboreshaji mfumo wa kocha na ulezi (coach and mentoring system) wa TRA ambao utawawezesha wafanyakazi wenye uzoefu na ujuzi wa TRA kuwafundisha na kuwalea wafanya kazi wapya wasio na uzoefu na ujuzi Eneo la tatu linahusisha uboreshaji wa mfumo wa mafunzo kwa wafanyakazi kupitia kuboresha mfumo wa ajira (career pathway manual) kwa wafanyakazi wa TRA.



Mafunzo ya wasimamizi wa programu ya kocha na ulezi (coach and mentoring)